

Na: Afg. 1443 H / 03

Jumapili, 07 Muharram 1443 H

15/08/2021 M

Taarifa kwa Vyombo vya Habari

Afghanistan Imo Ndani ya Majoribio ya Kihistoria baina ya Kusimamisha Khilafah au Kutabikisha Nidhamu Zilizotungwa na Wanadamu; Msipoteze Wakati Simamisheni Khilafah! (Imetafsiriwa)

Matukio ya ghafla na yasiyotabirika nchini Afghanistan kwa mara nyengine tena yameiweka nchi hiyo katika njia kwa vikundi anuwai vya kisiasa, viongozi wa kikabila na watu wenyewe ushawishi kufanya uamuzi juu ya mfumo wa kisiasa wa mustakbali nchini Afghanistan.

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir / Wilayah Afghanistan inawashauri viongozi wote wa kisiasa, washawishi wa kikabila, Mujahidina wa zamani, makundi anuwai, watu wenyewe nguvu kwamba nchi inapitia fursa ya kihistoria, inayowataka watu kukamata moja ya machaguo makuu mawili : 1) kusimamisha mfumo wa Mwenyezi Mungu (swt) kwa kurudisha Khilafah, na / au 2) kutabanni mfumo uliotengenezwa na wanadamu kwa kurudia hali ile ile chungu ya zamani.

Hivi sasa, Amerika, Ulaya, UN, na nchi za eneo zinashauriana na vyama anuwai vya kisiasa vya Afghanistan juu ya pendekeso la 'mfumo shirikishi', ambao utabeba viambishi vya Uislamu, kuzingatia sheria za Kimataifa, kujifunga na mipaka ya kitaifa na mchanganyiko wa Usekula na Uislamu, ambao ni lazima uidhinishwe na Jamii ya Kimataifa - mfumo ambao nyuso zingebadilika lakini sheria, nidhamu na muundo wa sasa zingebakia. Kunyakua aina kama hazo kumesababisha Afghanistan kutumbukia kwenye ukingo wa vita vya wenyewe kwa wenyewe, kutofaulu na kukwama kisiasa katika miongo michache iliyopita. Badala yake, Waislamu wengi wa Afghanistan wanatamani kusimamishwa kwa Dola ya Kiislamu na utawala wa sheria ya Kiislamu. Kwa hakika ni fursa nzuri, iliyopatikana baada ya miaka mingi ya mapambano ya kifakra, kisiasa na kijeshi dhidi ya uvamizi, na haipaswi kupotezwa na mawazo finyo na ukurupukaji, kitu ambacho kilipotea mara kadhaa kwa sababu ya makosa ya vyama vya kisiasa na watu wenyewe ushawishi.

Hizb ut Tahrir, kwa heshima ya dhati, kwa mara nyiningine tena inatoa wito kwa viongozi wote wa kisiasa, watu wenyewe ushawishi wa kikabila na makundi kukataa kata kata mapendekezo yoyote ya Amerika, UN, na nchi za eneo kuhusiana na mfumo wa kisiasa wa Afghanistan, na kutoruhusu kujitolea muhanga kwa Waislamu (ambako lengo lake lilikuwa ni kuregesha Sharia ya Kiislamu) kuharibiwa, bila kuleta matokeo yoyote yaliyotarajiwa. Badala yake, jaribuni kukusanya nguvu zenu kusimamisha mfumo wa Mwenyezi Mungu (swt) kwa kurudisha Khilafah - itumieni fursa ya sasa kwa ukamilifu! Kwa kweli, Afghanistan na eneo hili limekuza uwezo mkubwa wa kifakra, kisiasa, kiuchumi na kijeshi nyoyoni mwao, na endapo mfumo wa Mwenyezi Mungu (swt) utatabanniwa na kuitikiwa, In Sha Allah, mabadiliko makubwa yatafanyika katika pembe hii ya ulimwengu chini ya uongozi wa watu wanaofadhaika wa ardhi hii. Hii inahitaji watu wenyewe nguvu walio na imani na lengo kama hilo na waonyeshe uvumilivu dhidi ya shida kwa kutenda vitendo vyao kulingana na hukmu za Shari'a. Ni fursa kubwa kwa wale wanaotaka kuwa Ansar ullah (Wafuasi wa Mwenyezi Mungu) ya kusimamisha mfumo wa Mwenyezi Mungu, na kwa wale wanaotaka kutembea katika njia ya Maswahaba na kuchagua Jannah badala ya raha za muda za ulimwengu. Ni fursa kubwa ilioye hii kwa watu wenyewe hekima!

[يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِبُوْا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاهُمْ لِمَا يُحِبُّهُمْ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَحُولُ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَبْلِهِ وَأَنَّهُ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ]

"Enyi mlion amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hakika kwake Yeye tu mtakusanywa."

#Afghanistan

#Afghanistan

#Afghanistan

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Wilayah Afghanistan

Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir/Wilayah Afghanistan:

www.hizb-afghanistan.org

Pepe: info@hizb-afghanistan.org

Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:

www.hizb-ut-tahrir.org

Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:

www.hizb-ut-tahrir.info